**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA UCHUKUZI**

**MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI**

# TAARIFA KWA UMMA

## UTEKELEZAJI WA KANUNI – WASAFIRISHAJI KUAJIRI WAHUDUMU WA MABASI WALIOSAJILIWA NA LATRA

**Dodoma, Mei 17, 2025**

Kwa mujibu wa Kifungu cha 5(1)(e) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Sura ya 413, Mamlaka inajukumu la kusajili wahudumu na kuthibitisha madereva wa vyombo vya moto vinavyotoa huduma za usafiri kibiashara. Aidha, kanuni ya 22(g) ya Kanuni za Magari ya Abiria za Utoaji wa Leseni za Usafirishaji Tangazo la Serikali Na. 76 la Mwaka 2020, imeweka takwa la mtoa huduma kuhakikisha mhudumu anayemwajiri amesajiliwa na LATRA. Vilevile kanuni ya 20(1)(d) ya Kanuni za Uthibitishaji Madereva na Usajili Wahudumu wa Magari ya Biashara za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Tangazo la Serikali Na. 81 la Mwaka 2020 zinataka Mhudumu wa Magari ya kibiashara kuwa na Kadi ya Usajili iliyotolewa na Mamlaka.

Katika kutekeleza jukumu hilo, mwezi Julai 2023, Mamlaka ilizindua mafunzo ya wahudumu wa mabasi na tarehe 14 Agosti, 2024 Mamlaka ilitangaza tarehe 31 Disemba, 2024 kuwa mwisho wa watoa huduma nchini kutumia wahudumu ambao hawajasajiliwa na LATRA huku ikiendelea kutoa elimu na kuwezesha utekelezaji.

Hivyo, Mamlaka inawatangazia wamiliki na wahudumu wa mabasi ya kibiashara kwamba imeanza kukagua utekelezaji wa Sheria na Kanuni za udhibiti wa Wahudumu kwa mabasi yote ya masafa marefu. **Kuanzia tarehe 02 Juni, 2025 adhabu zitaendelea kutolewa kwa wanaokiuka Sheria hizo.**

Mamlaka inawakumbusha wahudumu wote kuwasilisha maombi ya kusajiliwa kupitia mfumo kwa rrims.latra.go.tz au kufika ofisi ya LATRA iliyokaribu wakiwa na nakala ya Cheti cha Mafunzo na namba ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA).

Mafunzo kwa wahudumu ni ya muda mfupi, yanatolewa na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), na Chuo cha Ufundi Arusha kwa utaratibu wa kuwafikia wahitaii.

Digitally Signed By Salum PAZZY
Sat May 17 02:54:17 EAT 2025

Salum PAZZY

**Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano**

LATRA Makao Makuu, S. L. P. 1742, 41104 Tambukareli, Dodoma
Simu + 255 262 323 930, Barua pepe: dg@latra.go.tz , info@latra.go.tz , Tovuti: www.latra.go.tz